JINA.................................................NAMBARI YA USAJILI..............

DARASA...........

**102/3**

**FORM 3**

**KISWAHILI**

**Muda: Saa 2½**

# SHULE YA UPILI YA SUNSHINE

# MTIHANI WA JULAI MWAKA 2019

KISWAHILI

Muda: Saa 2½

***Maagizo***

1) Jibu maswali manne
2) Maswali sharti yajibiwe kwenye nafasi zilizotolewa.
3) Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
4) Katika sehemu ya C, jibu swali moja.

*Kwa matumizi ya mtahini pekee*

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| FASIHI SIMULIZI | 20 | |
| KIGOGO | 20 | |
| TUMBO LISILOSHIBA | 20 | |
| USHAIRI | 20 | |
| | 100 | |

**TAMTHILIA KIGOGO** **(AL 20)**

"Naskia wanafunzi katika shule hizo zako hawafuzu. Wanaishia kuwa makabeji tu kwa kudungana sumu ya nyoka."

a) Eleza muktadha wa dondoo. (al. 4)

Ni maneno ya Ashua Akimwambia Majoka Ofisini mwa Majoka Wakati ambapo Majoka alikuwa anamkubusha kuhusu kazi katika shule ya Majoka and Majoka Academy.

b) Kwa kutolea mifano, taja mbinu mbili za lugha zilizotumika kwenye dondoo. (al. 2)

- Jazanda – Sumu ya nyoka
- Nahau – kuwa makabeji
- Utohozi – makabeji

c) Eleza sifa nne za mzungumumzaji wa dondoo (al 4)

- Mwenye hasira
- Mwenye tamaa
- Mwajibikaji
- Mwenye bidii
- Mtetezi wa haki
- Mwenye msimamo thabiti
- Ni mwaminifu
- Mwenye mapenzi

d) Jadili maudhui yoyote kumi katika tamthilia ya kigogo (al. 10)

Kazi
Elimu
Uongozi mbaya
Ufisadi
Ukatili
Tamaa/Ubinafsi
Vifo/Mauaji
Uwajibikaji
Madawa ya kulevya
Uzalendo
Uasherati
Mapenzi
Utetezi wa haki
Ubinafsi
Nafasi ya mwanamke
Ubabedume
Umaskini

## TUMBO LISILOSHIBA

Eleza changamoto zinazowakumba vijana katika elimu ukirejelea hadithi zifuatazo

a) Mapenzi kifaurongo (al 6 )

(i) Umaskini: Dennis anakosa mahitaji ya kimsingi kwa mfano Chakula

(ii) Ukosefu wa ajira: Vijana hawapati ajira baada ya kuhitimu masomoni.

(iii) Mapenzi ya kiholela: Dennis anawaona wanafunzi wenzake wakitembea wawili wawili kutoka Mashine Hall.

(iv) Utabaka: Dennis hawezi kununua vifaa vya thamani kama wenzake Kimani

(v) Kudhalilishwa na wahadhiri

(vi) Kutoelewa Masomo

b) Shogake dada ana ndevu (al 4)

i) Mimba za mapema: Safia anaambulia ujauzito akiwa Mwanafunzi wa Shule ya msingi.

ii) Uavyaji mimba: Safia anaenda kuavya mimba ili wazazi wake wasijue kuwa alipata ujauzito

(iii) Kutamauka: Safia anapogundua kuwa ni mjamzito, anakata tamaa na kuamua kuavya mimba.

(iv) Malezi mabaya: Wazazi wa Safia wanakosa kumakinika katika mienendo ya mwanao wanayemdhania kuwa ana maadili.

(v) Mapenzi ya Kiholela. Wanafunzi wanajiingiza katika mahusiano ya kimapenzi wakiwa Shuleni. Safia ana uhusiano wa kimapenzi na Kimwana.

c) Mama bakari (al 4)

i) Kubakwa/Kutengwa nyumba

ii) Kupuuzwa Shuleni

iii) Kutengwa na wanafunzi wenzako

(iv) Kupuuzwa nyumbani na wazazi

d) Mwalimu mstaafu (al 3 )

i) ~~Kufeli mitihani ya kitaifa~~ i) Kutoelewa masomo

ii) ~~Kutoelewa wanachofundishwa~~ ii) Ukosefu wa ridhaa

~~iii) Kupuuzwa~~ iii) Mapuuza

e) Mtihani wa maisha (al 3 )

i) Kufeli mitihani ya kitaifa

(ii) Kutoelewa wanachofundishwa

(iii) Kupuuzwa na walimu.

(iv) Kutamauka.

(v) Wazazi wakali

**Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali**

Ewe mainga wa Ndumi
Siwe uloambia akina mama
Siku tulopiga foleni
Chakula cha msaada kupata
Tuvulishe vifaranga kwenye miji
Wageuke vijusi tena
Njaa isiwaangamize?

Siwe ulopita
Matusi ukitema
Chumvi na sukari kutuvishia ja sumadi?
Ukatununu vihela ulotuvushia
Ukatununua kura ukapata?
Sasa miaka mitano imetimia
Waja tulaghai tena
Huna lolote safari hii
Ubunge umekudondoka ukitazama
Wanyonge tumeamua
Kwingine kujaribu

**Maswali**

i) Huu ni utungo wa aina gani. Dhibitisha (al 2)

Wimbo wa kisiasa
Kanunua kura.

ii) Eleza sifa nne za utungo huu (al 4)

1) Huwa na mwimbaji | waimbaji
2) Huweza kuambatana na ala
3) Huwa na urudiaji wa vifungu
4) Imejikita katika shughuli maalum
5) Huto sifa | kashfa za anayeelezewa
6) Huwa maudhui | mesuala yanayoikumba jamii

N.K.

iii) Eleza majukumu manne ya utungo huu (al4)

✓ Hukuza umoja wa kisiasa
✓ Huhamasisha watu
✓ Husawiri mfumo wa kisiasa na kijamii
✓ Husawiri mgogoro uliopo katika jamii
✓ Hutumiwa kueneza propaganda
✓ Huhimiza uzalendo na mshikamano wa kitaifa
✓ Hukashifu uongozi mbaya
✓ Huburudisha N.K

2. Chelewa chelewa utamkuta mwana si wako.

i) Huu ni uutngo wa aina gani? (al 1 )

methali

ii) Eleza sifa tatu za utungo huu (al 3 )

✓ Huwa ni fupi
✓ Huwa na sifa za kishairi
✓ Hujikita katika mazingira
✓ Huwa na sehemu mbili
✓ Huwa na tamathali nyingine za usemi
✓ Hueleza ukweli fulani katika jamii
✓ Huwa na maana ya ndani na ya nje

3. i) Tofautisha kati ya mighani na ngano za mashujaa (al 1)

Mighani ni hadithi za kweli za mashujaa
uhali ngano za mashujaa ni za kubuni

ii) Toa neno mwafaka kwa maelezo yafuatayo

a) Maelezo kuhusu matukio ya kihistoria kulingana na yalivyofuatana ki wakati (al 1)

Tarihi

b) Hadithi ambapo mhusika hukabiliwa na hail ngumu ya kuamua baina ya mambo mawili au Zaidi yanayomkabili (al 1)

Ngano za mtanziko

c) Tambua vipera sita vya maigizo (al 3)

| | | |
|---|---|---|
| michezo ya jukwaani | Ngonjera | ngomezi |
| Vichekesho | Ngoma | |
| Majigambo \| vivingo | Mwiga | |
| michezo ya watoto | Metambila | |

**USHAIRI**

**Soma shairi hili kisha ujibu maswali**

El-nino, harufuyo yatughasi, tangazo lako, ni vilio huvileta.
El-nino, hushtushwa na unyasi, ambaye nyoka, awali alimng'ata
El-nino, vua tesi la nafusi, maafa yako, hayatupaki mafuta.

El-nino, mno tuna wasiswasi, mahangaiko, ukija tatakipata
El-nino, hayo hutufika nasi, tukatoroka, nyumba zetu zikajeta
El-nino, wewe na vyako vikosi, mkitufika, mno hutupa kusota.

El-nino, mbiu yako iko nasi, washatangaza, waanza kututafuta
El-nino, tangazo tumeliasi, unavyotuliza, hutakiki katakata
El-nino, hatuamini ni sisi, utatuliza, kila mahali kutota.

El-nino, dunia huitakasi, waangamiza, nyumba zikakosa kuta.
El-nino, mafuriko ni vifusi, yatabakiza, kibomoka hizo kuta
El-nino, utawasomba farasi, mbu kujaza, na maradhi kutupata.

El-nino, twambwa mvua Baraka, lakini yako, tesi sisi kitupata
El-nino, makazi huvurugika, kila ujako, na miji ikazorota
El-nino, wengi wakilipulika, latajwa lako, mawazo huwavukuta.

El-nino, kwa wengine ni mrija, fedha za uma, mbawa zipate kuota
El-nino, wakisikiya ukija, visu vya nyama, kwa usafi huvifuta
El-nino, ni lini 'taleta tija, kwa mkulima, awe bure hakupata?

**MASWALI**

a) Hili ni shairi la aina gani. (al 1)

..........................................................................................................

b) Onyesha hali hasi ambazo nafsineni anazitaja katika shairi hili (al 3)

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

c) Tofautisha ujumbe katika ubeti wa pili na wa mwisho (al 1)

..........................................................................................................

..........................................................................................................

d) Onyesha jinsi mshairi alivyotumia kibali chake (al 4)

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

# MASWALI

a) Hili ni shairi la aina gani? (alama 1)
tathlitha - lina mishororo mitatu katika kila ubeti

b) Onyesha hali hasi ambazo nafsinene anazitaja katika shairi hili (alama 3)
hali hasi - hali ambazo hazipendezi / zinazoleta maangamizi
i) Elnino huletesa nafsi za watu
huleta mahangaiko
hufanya watu watoroke makwao
husababisha mateso kwa waja
hubomoa nyumba
husomba mifugo kama farasi, mbuzi n
huvuruga makao yakibaribika

c Tofautisha ujumbe katika ubeti wa pili ~~wa~~ za na wa mwisho. (alama 2)
ubeti 1 - unaonyesha kuwa El-nino inaleta maafa, mahangaiko ~~na~~ wasiwasi. kwa watu, watu hutoroka kwao
ubeti 6 - El-nino inaleta faida na watu wanajipatia fedha za umma na inakuwa ni chanzo cha kutajirika.

d Onyesha jinsi mshairi alivyotumia kibali chake. (alama 3)
Inkisari harufuyo - harufu yako
twambwa - twaambiwa
taleta - utaleta
Mazida wakilipulika - wakipulika hulakiki - hulak
lahaja wakipulika - wakisikiliza
Tabdila [illegible]

Kubonga isarufi
vyako vikosi - vikosi vyako
mno hutupa kusota - hutupa kusota mno
ambaye nyoka awali alimmeza - nyoka
ambaye alimmeza awali

e Onyesha aina za taswira zilizotumiwa katika shairi (alama 2)
Taswira mnuso - harufu ya el-nino
" ya mwendo - watu kuhangaika, watoroke - wasomba farasi mbuzi.
" oni - kuta za nyumba kubomoka nyoka alimmeza
usikivu/kusikiliza - watu wakisikia Elnino ikija

f Eleza mbinu za lugha zilizotumiwa katika shairi (alama 2)
maswali ya balagha - awe bure hakupata
Tashhisi - El-nino imepewa uwezo wa kutangaza kupiga mbiu, uwezo wa kutaputa binadamu, kuwa utesi

g Tambua bahari za shairi hili ukizingatia;
i mpangilio wa maneno (alama 3)
Kikwamba
ii mpangilio wa vina
Ukara - vina vya mwisho vinatiririka
iv mizani wa vipande
Bamba/Tuo - vipande vinne

h) Andika ubeti wa pili kwa lugha tutumbi (alama 4)

Elnino inapokuja watu huathirika sana huwa na wasiwasi na kuhangaiko. Husababisha watu kutoroka nyumbani baada ya nyumba zao kubomolewa. Elnino inapowashambulia watu na vikosi ~~wake~~, husababisha maumivu mengi.

i) Eleza maana ya mleo wa ~~wa~~ ukingo wa ubeti wa tano (alama 1)

mawazo huwavukuta - mawazo mazito ya kuumiza akili.